**Muhtasari wa Kikao cha Ushirikiano wa Jumuiya wa DOH**

Mwezi wa Disemba 20, 2023 | 3:30 jioni – 5:00 jioni PT

## Kukaribisha Watu na Utambulisho

Amelia Bai, ambaye ni Mshirika wa Mawazo ay Ushirikiano wa Jumuiya na Mwezeshaji Mwenza wa Kikao, amewakaribisha wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya kwa kikao.

Walohudhuria kikao hicho walijitambulisha katika Gumzo (*Chat*).

Amelia amesema kuwa mkutano ulikuwa unarekodiwa kwa usahihi na kufanya majadiliano ya mkutano yapatikane na wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya ambao hawakuwa kwenye mkutano, na kwamba kurekodi kunaweza kusimamishwa wakati wowote wakati wa mkutano kulingana na matakwa ya Ushirikiano wa Jumuiya. Alibainisha kuwa faraja na ufaragha wa wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya ndiyo maswala yao makuu wanayoyataka kuyahakikisha, na kwamba wanajitahidi kudumisha nafasi salama kwa sauti zote za jumuiya.

## Ufikiaji & Uelekezaji wa Zoom

Tom Dineen, ambaye ni Mwezeshaji wa Teknolojia wa Shirika la Kauffman and Associates Inc (KAI), alikagua vipengele vya Zoom na kueleza jinsi ya kutafuta usaidizi wa kiufundi/lugha wakati wa mkutano.

Licha ya Kimomba kutumiwa, lugha hizi zingine zilitumika kutafsiria na kupata maelezo wakati wote mkutano ulikuwa unaendelea:

- Lugha ya Ishara ya Marekani
- Kichina (*Mandarin*)
- Maelezo ya picha zinazoonyeshwa ndani ya kompyuta
- Kikorea
- Kireno
- Lugha ya Kirusi
- Kihispania
- Kiswahili
- Kivietinamu

## Mapitio ya Ajenda na Mambo ya Ardhi

Amelia amepitia ajenda na akasoma mambo ya Ardhi & Kazi (tazama slaidi za kompyuta (*slides*) za mkutano ili kupata maelezo mengi).

## Maelezo Juu ya Mahusiano ya Jumuiya: Pendekezo la Gavana la Bajeti ya Nyongeza ya 2024

Elizabeth Perez, Mkuu wa Ofisi ya Mtendaji wa Masuala ya Umma na Usawa, Idara ya Afya ya Jimbo la Washington (DOH), alitoa maelezo yanayofuata ya haraka haraka ambayo ni mapya na kuhusiana na pendekezo la Gavana la bajeti.

- Miezi kadhaa iliyopita, Kelly Cooper aliwasilisha kwa Jumuiya ya Ushirikiano kuhusu mapendekezo ambayo DOH ilikuwa ikitoa, na wiki iliyopita, Gavana alitoa bajeti yake ya ziada (https://ofm.wa.gov/budget/state-budgets/gov-inslees-proposed-2024-supplemental-budgets). Elizabeth alifafanua ya kuwa bajeti ya ziada ya Gavana itapitia kikao cha sheria na mambo yanaweza kubadilika. Kikundi cha Uhusiano na Usawa cha DOH kiliwasilisha Jumla ya Uamuzi unaohusiana na Ushirikiano wa Jumuiya na ushiriki wa jumuiya. Kiasi cha dola kilijumuishwa na mipango mingine michache ya usawa, na ilikuwa takriban $4 au $5 milioni. DOH ilipata bajeti ya Gavana karibu dola 200,000 ambazo alikuwa ameweka kwa ajili ya mipango hiyo. Baadi ya mambo muhimu yaliyojumuishwa kulikuwa na ufadhili ambao ulitengwa kwa laini ya kuzuia ya siku 90 ya DOH ili kusaidia na maswala ya miundombinu ambayo yanaendelea kutokea na hiyo ni njia ya kuzuia kujiua. Pia kuna baadhi ya dola au pesa zilizotengwa kwa mradi wa kupambana na *opioids*. Ilikuwa ni kipaumbele cha Gavana, na ilikuwa takriban dola milioni 69. DOH inakaribia kupata dola milioni 4 kati ya hizo na $3 milioni kwa kampeni ya taarifa kwa umma. DOH iliendesha kampeni ya taarifa kwa umma wakati wa kiangazi kuhusiana na kupunguza tatizo ndani kwa kutumia dawa ya *Naloxone* (dawa ya kuokoa maisha ya aliyekula *opioids* kupitia kiasi), na itakuwa mwendelezo wa juhudi. Kuna ufadhili Fulani ambao uliingia katika kusaidia kukamilika kwa teknolojia ya DOH, na ufadhili fulani uliingia katika mipango mingine ya usawa kuhusiana na hasa Sheria ya HEAL na mambo ya Usawa wa Afya. Elizabeth alifafanua ya kuwa baadhi ya mapendekezo ambayo DOH ilitoa na hayakupata ufadhili, ni mradi wa chanjo wa Care A Van (chanjo za mbua na paka za kupelekwa na gari nyumba za watu), chanjo za watu wazima, na mipango mingine. Timu ya DOH itaendelea kurejea kwa Ushirikiano wa Jumuiya ili kutoa taarifa zaidi kuhusu kile kinachoendelea na ambapo DOH inaendelea kupiga hatua katika mchakato wa bajeti. Alibainisha kuwa kwa ujumla, Gavana aliweka mambo muhimu na vipaumbele vyake kuzingatia ukosefu wa makazi, mabadiliko ya hali ya hewa, janga la *opioid*, na elimu.(https://ofm.wa.gov/sites/default/files/public/budget/statebudget/highlights/budget24/00_24_Budget-Policy-Highlights.pdf).
- Elizabeth alibainisha kuwa mapendekezo yote ambayo DOH ilitoa kwa bunge katika ofisi ya Gavana ni taarifa ya umma na yanapatikana kwa umma kusoma kuhusu vipaumbele vyao na nini wanaomba fedha kwa ajili ya kazi ambayo wanajaribu kufanya (https://doh.wa.gov/about-us/budget-contracts-and-grants/budget-information/2023-25-budget-proposal).

Elizabeth alibainisha kuwa watarudi kwenye Jumuiya ya Ushirikiano ili kutoa sasisho baada ya kikao cha sheria ili kuona nini kitatokea, kutoka kwa yale ambayo DOH iliwasilisha hadi yale ambayo Gavana aliwasilisha na kwa kile ambacho kwa kweli Bunge linafadhili.

## Ushirikiano wa Jumuiya: Mapitio ya Mwanzo wa Mwaka

JanMarie Ward, Mshirika wa Mawazo na Mwezeshaji Mwenza wa Kikako aliangazia mafanikio yafuatayo ya Ushirikiano wa Jumuiya yaliyopatikana katika mwaka wa 2023 na fursa zilizopo kuelekea mbele. Ili kupata maelezo ya ziada, tafadhali kagua slaidi za uwasilishaji.

- JanMarie alifafanua kwanza ya kuwa Ushirikiano wa Jumuiya unalenga na kuzingatia kuhakikisha sauti za jumuiya zinasikika na kuingizwa katika kufanya maamuzi kwa sera, programu, na uwekezaji wa jumiya ili kushughulikia usambazaji sawa wa chanjo na ufikiaji wa juhudi za juu za kukabiliana na janga. Alibainisha ya kuwa mwaka huu umekuwa mwaka wa kusitisha mambo na wa mpito na Ushirikiano umeweza kubadilisha jina lake toka Ushirikiano wa Utekelezaji wa Chanjo hadi Ushirikiano wa Jumuiya ili 1) kupanua lengo ili kujumuisha masuala ya kupona kwa muda mrefu na kupunguza masuala yanayohusiana na uthabiti na kushughulikia ubaguzi wa kimfumo kulingana na rangi ya watu na ukandamizaji, ambao uliongezwa wakati wa janga; na 2) kuimarisha muundo wa ndani wa Ushirikiano (mfano, kutambua ufadhili wa mkandarasi wa usaidizi wa kiufundi ili kusaidia kutoa programu na usaidizi wa vifaa kwa ajili ya kazi inayoendelea ya Ushirikiano; kutumia Tovuti ya WA Portal ili kuwawezesha washirika kuunganishwa, kuongeza raslimali na kunufaika kutokamana na raslimali, na kuwezesha fursa mpya za ushirikiano).
- Mnamo 2023, Jumuiya ya Ushirikiano iliweza kuandaa Vikao 6 vya Ushirikiano wa Jumuiya, mikutano 14 ya Washirika wa Mawazo, mikutano mingi ya Kikundi cha Kazi, na mikutano mingi yasiyofuata jadwali rasmi au ukipenda *Ad Hoc meetings* kwa Kimombo.
- Ushirikiano wa Jumuiya pia ulisikia Muhtasari mwingi wa Mahusiano ya Jamii, ambao uongozi wa DOH ulitoa maelezo juu ya mada anuwai, kwa mfano:
    - <u>Mwisho wa Dharura ya Afya ya Umma na Ushirikiano wa uongozi wa DOH.</u> Wakati wa kikao, uongozi wa DOH ulishiriki mawazo, ulitoa shukrani kwa juhudi za jumuiya, ulishiriki majadiliano na jumuiya, na baadaaye ulirekebisha mambo kuwa na Afisa wa Usawa kama sehemu ya timu ya Usimamizi wa Matukio.DOH itaendelea kuhakikisha kuwa sauti za jumuiya zinasikika. JanMarie alibainisha kuwa wakati wa COVID-19 ulikuwa mara ya kwanza DOH kupokea ufadhili wa ushirikiano wa jamii ili kukabiliana na dharura, ambayo ni mabadiliko ya kiwango cha mfumo. Zaidi ya hayo, wakala umekuwa ukitafuta njia za kuboresha ukandarasi na umefanya maendeleo ya kiutawala katika suala hilo. Kwa upande wa ufanisi na michakato, DOH imeanzisha Mpango wa Njia za Wafanyakazi ili kuelekea kufikia nguvu kazi ambayo inawakilisha zaidi jamii. DOH imejitolea kutafuta njia za kuendeleza juhudi za kuimarisha uwezo na kuendelea kushirikisha jamii. Mpango wa Mabadiliko umeweka vipaumbele

(https://doh.wa.gov/about-us/transformational-plan), na Ofisi ya Sera, Mipango, na Tathmini ina ofisi mpya inayozingatia utendakazi na uwajibikaji.
   - Ugonjwa wa COVID wa kuendelea muda mrefu. Jumuiya ya Ushirikiano ilishirikiana na Afisa Mkuu wa Sayansi wa DOH na kujifunza kuhusu Ugonjwa wa COVID wa kuendelea muda mrefu au COVID ya muda mrefu, kama vile ishara, dalili, matibabu na chanjo.
   - Mwezi wa Maandalizi ya Kitaifa: Maandalizi ya Jumuiya. Kipaumbele hiki pia kinasisitizwa katika Mpango Mkakati wa Mabadiliko wa DOH.
   - Maelezo Mpya ya Mpango wa Chanjo ya COVID-19 na Kubadilika kwa Mandhari ya Chanjo za COVID-19. Mnamo mwaka wa 2023, chanjo zimekuwa zinatolewa kibiashara badala ya serikali ya shirikisho kuzigawa. DOH inaendelea kutoa taarifa mara kwa mara kuhusiana na Mpango wa Upataji wa Daraja la Shirikisho ili ku hakikisha upatikanaji wa chanjo.
   - Msimu wa Chanjo ya Virusi Vinayodhuru Mfumo wa Kupumua na Maelezo Mapya ya Chanjo. Timu za DOH zimetumia chati au *charts* na dashibodi ili kuonyesha viwango vya chanjo katika Jimbo lote na miongoni mwa jamii mbalimbali na makabila. Kazi inaendelea katika suala hilo. DOH imeshiriki raslimali, na jumuiya inaendelea kupokea maelezo mapya kuhusu chanjo kama vile Care-A-Van.

JanMarie aliangazia mipango ifuatayo ambayo Ushirikiano ulitoa maoni mnamo 2023 na utaendelea kusikia zaidi mnamo 2024:

- Sheria ya HEAL na Harakati ya Haki ya Mazingira, ambayo inalenga katika kuboresha afya ya wakazi wote wa jimbo la Washington na kuboresha hali njema na ubora wa Maisha kwa jamii za rangi au wasiokuwa Wazungu na kaya zenye kipato cha chini kote jimboni kwani uchafuzi wa mazingira unaathiri kwa kiasi kikubwa jamii za rangi au wasiokuwa Wazungu na jamii asili. DOH itatekeleza SHERIA YA HEAL kupitia ushirikiano wa jamii,mashauriano wa Makabila, Mpango Mkakati wa EJ IN, tathmini za EJ, na upangaji bajeti na ufadhili wa EJ IN, na lengo ni kubadilisha utamaduni wa wakala, sera na utendaji. Hii ni kazi inayoendelea, na jumuiya itajifunza zaidi kuihusu mwaka wa 2024.
- Mpango wa Usawa na Kupinga Ubaguzi wa Rangi (PEAR) na Kitabu cha Mchezo au Tamthilia. Madhumuni ya PEAR ni kukuza mazingira ambayo yanaunda kumilikiwa na kuanzisha utamaduni wa kuunga mkono usawa na kupinga ubaguzi wa rangi kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA) na watu wanaofanya kazi nao na kuwahudumia. Kila shirika la serikali lina jukumu la kuunda mpango wao maalum. PEAR ni sehemu ya kazi ya HCA, na baadhi ya wanachama wa Ushirikiano wameshiriki katika kazi ya Timu ya Ushauri ya Jamii ya PEAR (CAT).
- Jumla ya Mapendekezo ya DOH ya Uamuzi wa Kisheria na Sheria ya Ombi la Wakala. Kulikuwa na vifurushi 15 vya uamuzi wa awali kutoka DOH. DOH imeshiriki mpango wake wa kushirikisha Jumuiya na kufanya mazungumzo ya kina zaidi kwa Kikao cha Sheria cha 2025. Kuanzia mawanzoni mwa 2024, Jumuiya kwa kweli itaanza kujihusisha kwenye Kikao cha Sheria cha 2025.

- Jumla ya Mapendekezo ya Uamuzi wa Awali: Care-A-Van, kampeni ya vyombo vya habari inayoangalia nje, chanjo za watu wazima, kuendeleza mpango wetu wa Care Connect Washington, kutekeleza mpango wa PEAR (Pro-Equity Anti-Racism) na fidia ya jamii, Mpnago wa Ruzuku wa Mambo ya Usawa wa Afya (HEZ), uwekezaji katika teknolojia ya habari, ikiwemo *Informatics* (kujua mambo ya habari) na Teknolojia ya Afya ya Umma, na uwekezaji katika Utekelezaji wetu wa Huduma ya Afya na Mfumo wa Usimamizi wa Utoaji wa Leseni (HELMS)
    - Kikao cha Sheria cha 2024 kilianza kwa DOH kuandaa maobi ya bajeti na ajenda ya kisheria mnamo mwezi wa Mei hadi Julai 2023, maelezo ya ziada yakijumuisha:
        - DOH ilishirikisha jamii na washirika katika muda wote wa Agosti 2023
        - DOH ilifanya mikutano mitandaoni yaani *webinars* Agosti 28, 2023
        - Mapendekezo ya DOH ya 2024 yalitolewa kwa ofisi ya Gavana mnamo Septemba 13, 2023
        - Kikao cha Kisheria cha 2024 kitaanza tarehe 8 Januari, 2024
        - Mwisho wa Kikao cha Sheria ni tarehe 7 Machi, 2024
- Utofauti katika Majaribio ya Kiafya. Washirika wa Fikra au Mawazo waliangazia mswada (2 SHB 1745) kuhusu kuboresha utofauti katika majaribio ya kimatibabu na wakashiriki muktadha wa kihistoria, wakibainisha madhara yaliyosababishwa ambayo yalisababisha kutoaminiana. JanMarie alibainisha kuwa kuna ripoti inayosubiriwa na Ushirikiano unatazamia kuona matokeo ya ripoti hiyo.
- Mpango wa Mabadiliko wa DOH. Mpango huo unazingatia masuala 5 ya kipaumble: Afya na Ustawi, Mifumo ya Afya na Mabadiliko ya Nguvu Kazi, Afya ya Mazingira, Mwitiko wa Dharura na Ustahimilivu, na Afya ya Ulumwenguni na Mtu Mmoja Mmoja. JanMarie alihimiza Ushirikiano wa Jumuiya kufanya kazi Pamoja ili kutafuta njia za kuendeleza juu ya kile ambacho kimefanywa, na kufaidika kutokamana na fursa za kuendeleza kazi mbele. Alibainisha kuwa Ushirikiano wa Jumuiya ulishiriki katika mijadala mifupi na kushiriki vipaumbele vyao kuhusu kile kilichokosekana.
- Uhamasishaji Unaoendeshwa na Jamii. Ushirikiano wa Jumuiya pia ulisikia kuhusu Mpango wa Uhamasishaji unaoendeshwa na Jumuiya ya DOH na ukajifunza na kuhusu juhudi za mashirika ya kijamii ili kuhakikisha ufikiaji wenye usawa zaidi wa taarifa za COVID-19, rasilimali, na chanjo huku ikishughulikia viambatisho vya kijamii vya afya. Ushirikiano na DOH zitaendelea kushirikiana na mashirika pamoja na Washirika wa Wahindi wa Mijini na watakuwa wakisikia kuhusu kazi yao inayoendelea katika miezi michache ijayo na watatoa maoni.

    - Wanakandarasi/Washirika wa Uhamasishaji Unaoendeshwa na Jamii: shirika la APARTNERSHIP, kituo cha utamaduni cha ASIA PACIFIC CULTURAL CENTER, kituo cha utamaduni cha CENTRO CULTURAL MEXICANO, kituo cha CENTER FOR MULTICULTURAL HEALTH, COMAGINE HEALTH, Desautel Hege (DH), mradi wa Health Commons Project, washirika wa Momentum Professional Strategy Partners, Huduma za Wakimbizi na Wahamiaji wa Kaskazini-Magharibi (RISNW), shirika la Yakima Valley Community Foundation (YVCF)

- Washirika wa Mawazo. JanMarie alifafanua ya kuwa Washirika wa Mawazo ni wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya ambao huchukua majukumu rasmi zaidi na Ushirikiano wa Jumuiya; wao wanafanya kazi kama bodi ya ushauri, huongoza mwelekeo ndani ya upeo wa Ushirikiano, na kutoa mwongozo na maarifa kwa DOH ili kuhakikisha kwamba Ushirikiano unaongozwa na jamii na unazingatia juhudi zinazoongozwa na jumuiya. JanMarie aliangazia kazi ifuatayo amayo Washirika wa Mawazo wamekamilisha mnamo 2023:
    - Kijitabu na ripoti ya Maelezo ya COVID-19, ambayo itatolewa mwaka ujao.
    - Walitoa majibu yanayohusu Miongozo ya Fidia ya Jumuiya ya DOH, ambayo ni kazi inayoendelea.
    - Walishiriki katika majadiliano kuhusu Utawala Sawa katika Mifumo ya Afya na Uhakikisho wa Ubora, ambao utainua sauti ya jamii.
    - Mikutano isiyofuata jadwali rasmi au Ad hoc ya kupanga mambo iliyoandaliwa kwa ushirikiano na DOH na kuhusiana na 2SHB 1745, ambayo kwayo Washirika wa Mawazo walitoa muktadha wa kihistoria.
    - Kushiriki kwa mtandao mkutano wa *webinar* wa Washirika wa Sheria
    - Walitoa maoni kuhusu fursa za ufadhili za DOH, ikiwa ni pamoja na majaribio ya tathmini ya haki ya mazingira ili kutambua jamii zilizoathiriwa zaidi na fursa za ruzuku ndogo za jamii.
    - Walishiriki katika kamati za ukaguzi ili kuchagua mashirika 43 ya kijamii ya kufadhiliwa kama sehemu ya Kujenga Uwezo Wa Jamii Kwa Fursa Sawa Ya Ufadhili Wa Uponyanji Kutokamana Na Ugonjwa Wa COVID-19.
    - Wameshiriki katika riwaya na utafiti wa tathmini ya mazoea ibuka juu ya mbinu ya ufadhili sawa na mtandao wa kitaifa wa taasisi za afya ya umma na Chuo Kikuu cha Michigan.
    - Wameshiriki katika Wasifu wa Kila Siku wa DOH na Vivutio vya Afya ya Umma, vinavyoangazia jamii na kushiriki mitazamo ya viongozi wa jamii.
    - Walitoa mwongozo na maoni kuhusu Utawala wa Ufadhili Unaopewa Mnufaika Mpya Kila Wakati wa Maji ya Kunywa
    - Walishiriki katika Majopo ya DOH ya Usaili Wafanyakazi Wapya na walihusika katika michakato ya kuwaajiri

- Walianza kupanga juu ya maendeleo ya Tathmini ya Ushirikiano wa Jumuiya ili kubaini vipaumbele na mwelekeo wa siku zijazo wa Ushirikiano ili kufahamisha majadiliano ya upangaji mkakati.

- Walikuza uelewa katika masuala mengine mengi, ikiwa pamoja na Harakati Huru za Maisha yaani *Independent Living Movement*, Usawa wa Afya wa Carceral Health Equity (afya ya wafungwa hasa), na miunganisho na mashirika mengine na washirika ili kuendeleza usawa.

JanMarie alipeana maelezo ya ziada kuhusu uwakilishi wa Ushirikiano wa Jumuiya mnamo 2023:

- Uanachama: Jumla ya wanachama 827 walosajiliwa wakiwemo wanachama 255 ambao ni wanachama hai au wanaofanya kazi kwa ratiba ya kawaida kwa bidii. Mnamo 2023, watu 572 wa Ushirikiano wa Jumuiya wamefikiwa, na uhamasishaji umezua shauku na ushiriki unaoendelea.
- 
- Mahudhurio: Ushiriki wa Kikao cha Ushirikiano wa Jumuiya umekuwa ukiongezeka mwaka mzima, kutoka 74 Mei hadi 108 mwezi wa Oktoba.
- 
- Uwakilishi wa kijiografia: Ingawa kuna uwakilishi katika Jimbo lote, kuna fursa za kufikia maeneo ya vijijini katika suala la ushiriki.
- 
- Walohudhuria na kujitambulisha na ragi/makabila yao kwa hiari yao: Wengi miongoni mwa walohudhuria katika Vikao vya Ushirikiano wa Jumuiya hawakujitambulisha. JanMarie alipendekeza kwepo mzungumzo kuhusu mada hii.

    - Todd alisisitiza ya kuwa tunahitaji kuhakikisha tunapata au kufahamu hesabu kwa usahihi. Yeye alieleza umuhimu wa uwakilishi ili kuhakikisha sauti zetu zinasikika, hasa wakati Ofisi ya Sensa na Bunge la *Congress* kufanya kazi zao utakapowadia.

- Lugha za walohudhuria: Fauka ya Kimombo, kuna lugha zingine za waliohudhuria. JanMarie alikuwa anataka kujua iwapo walohudhuria walipeana maelezo kuzihusu lugha ambazo wanazipendelea zitumike.

**Majadiliano/Maoni**

- Mtu mmoja ambaye ni miongoni mwa walohudhuria mkutano aliuliza hivi kwenye sehemu ya mazungumzo ya *Chat*: “Je tuna idadi ya watu kutoka slaidi (*slide*) iliyotangulia iliyogawanywa kulingana na umri?”
    - Gillissen ambaye ni kutoka KAI alijibu “hatuulizi umri wa mtu katika fomu ya usajili. Maelezo yote yamekusanywa kwa kutumia fomu ya usajili. Lakini kwa

kusema kweli tunaweza kuyachukulia maswali nyuma ili tujadiliane tukiwa tunayaongeza."

- Mtu mmoja mwingine miongoni mwa walohudhuria aliuliza hivi: "Badala ya umri halisi wa mtu, je, tunaweza kuwauliza walohudhuria wote umri wao ni kuanzia miaka ngapi hadi miaka ngapi kwa jumla?"

- Todd alishiriki mifano katika *Chat* ili kuangazia kwamba Ofisi ya Sensa inahitaji maoni ya jumuiya: https://ndrn.salsalabs.org/censusdisability/index.html?link_id=0&can_id=1e4a9cc154d58cff6ad746bad4c40a89&source=email-action-alert-its-not-too-late-ask-budget-writers-to-fund-critical-supports-for-students-in-crisis-2&email_referrer=email_2149751&email_subject=action-alert-tell-the-census-bureau-nothing-about-us-without-us
- Todd alishiriki pia mfano wa jibu kutoka mshirika wa kitaifa ambaye ana mahusiano na wao na WA DOH na hata Maisha Huru au *Independent Living*: https://disasterstrategies.org/comments-on-proposed-changes-to-american-community-survey-including-prcs/
- Mhudhuriaji wa mkutano alitoa maoni kwenye sehemu ya mazungumzo ya Chat: "Mimi ni mpya hapa, lakini kusema kweli nimefurahi sana kujua afya ya Mazingira iko mezani kujadiliwa na nataraji kuwa nitasikia/au kujua mengi juu yake na kujumuishwa hiyo kwa kazi yetu."

## Maelezo ya Kikundi cha Kazi

Kufuatia Mapitio ya Mwaka Ulioanza sasa, Vikundi 3 vya Kazi vifuatavyo vilishiriki maelezo mafupi.

**Kikundi cha Usawa cha Afya cha Hawaii/Kisiwa cha Pasifiki:**

- Viongozi Wenza: Tausili Kalepo na Ala Talo
- Matukio ya Mkutano: Jumatatu ya Kwanza ya kila mwezi saa 3:30-5:00 jioni (kwa sasa yamesitishwa lakini yataanza tena 2024)
- Maelezo ya kikundi cha kazi:
  - Vipaumbele vya sera vya Wakazi wa Visiwa vya Pasifiki
  - Kazi kusonga mbele

Tausili alitoa shukrani kwa kupata nafasi hiyo ambapo wameweza kujadili masuala ya kisera. Alieleza kuwa tangu alipoanza kazi kama mwezeshaji mwenza wa mkutano mnamo mwezi wa tisa 2023, kikundi hicho kilitaka kufanyia kazi mikakati ili waweze kufanya mabadiliko ya sheria. Katika mikutano ya mwezi wa tisa na Oktoba, kikundi kilibainisha masuala 3 bora ambayo wao na mashirika ya jamii (CBOs) wanafanya kazi nayo wanataka kuzingatia, yakiwa ni pamoja na makazi, afya ya kinga, na afya ya akili kwa watu wazima wenye umri mdogo bado na vijana. Tausili aliyaita mashirika ya CBOs wanayofanya kazi nayo na Bodi ya Afya ya Wakazi wa Visiwa

vya Pasifiki, Kituo cha Utamaduni cha Asia Pacific, Jumuiya ya Wakazi wa Visiwa vya Pasifiki vya Washington, Utopia, Muungano wa Afya wa Wakazi wa Visiwa vya Pasifiki Kaskazini Magharibi, na sauti za Pasifiki ya Kusini. Tausili alieleza kuwa katika mkutano wao wa Novemba, walifanya mazungumzo ya jamii na kiongozi wa jamii kutoka Jumuiya ya Wakazi wa Visiwa vya Pasifiki ambaye aliwasaidia kuibua mambo mengi zaidi, na kutakuwa na ripoti itakayotoka hivi karibuni, ambayo watashiriki na DOH na washirika wengine wanaojiunga mwito wao wa kila mwezi. Mikutano ya kikundi kwa sasa inasimamishwa kwa sababu mashirika ya CBOs yanafanya kazi nyingine nyingi, na yanataka kukusudia kuhusu masuala ambayo yangependa kuzingatia. Tukitarajia mambo mema kwenye mustakbali, kikundi kinapanga kurejesha mazungumzo yake mapema 2024 ili kukagua mikakati na kutathmini kazi kinachoweza kufanya ili kuendelea kuleta matokeo chanya.

Ala alitoa shukrani kwa kuwa sehemu ya Ushirikiano wa Jumuiya na aliwashukuru Frances na Juliet kwa msaada na mwongozo wao.

**Kikundi cha Kazi cha Usawa wa Afya ya Carceral (yaani afya ya wafungwa)**

- Viongozi Wenza: Cyril Walrond na Omid Bagheri Garakani (DOH)
- Matukio ya Mkutano: Jumanne ya Pili ya kila mwezi 3:00-5:00 jioni
- Maelezo ya kikundi cha kazi:
    - Kikundi kipya cha kazi kilichoanzishwa kilizingatia madhara ya kiafya ya mfumo wa carceral (yaani mfumo wa afya ya wafungwa)
    - Ushirikiano kati ya washirika wa jumuiya na wafanyakazi wa DOH wanaoongoza kazi mpya inayotekelezwa HB 1470

Cyril Walrond alibainisha kuwa Kikundi hiki cha Kazi ni nafasi ya ushirikiano iliyoundwa na watu wengi kutoka Kundi la Jumuiya ya Wafungwa Weusi ambao wanapanga masuala haya ndani na nje ya nafasi. Kundi la Jumuiya ya Wafungwa Weusi lina historia ya kuandaa aina hizi za masuala tangu 1972, na kwa miaka mingi kazi yao imesababisha mabadiliko makubwa ndani ya mfumo wa *carceral* wa afya ya wafungwa.Cyril alielezea kuwa Kikundi cha Kazi cha Usawa wa Afya cha Carceral kiliundwa wakati wa janga la COVID-19, ambalo liliangazia tofauti kubwa za kiafya ambazo zinaathiri wanajamii waliofungwa.Alibainisha kuwa Kikundi cha Kazi kimejitolea kuzingatia usawa ili kushughulikia sera, mazoea, na ufadhili ambao unaathiri afya ya wanachama waliofungwa.Cyril alielezea kuwa wanatumai pia kuunda nafasi kwa jamii kusimamia mambo tofauti ambayo yanahitajika ili kuathiri mabadiliko katika Jimbo zima, na kushirikiana na DOH. Alibainisha kuwa Kikundi cha Kazi kinatazamia kuona na kufanya mambo ambayo yataleta mabadiliko. Akirejelea uungwaji mkono wa mwanachama wa Baraza la Wafungwa Weusi ambaye amegunduliwa hivi majuzi na saratani ya hatua ya 4, Cyril alidokeza kukosekana na kucheleweshwa kwa upatikanaji wa huduma za afya katika mfumo wa carceral.Alibainisha kuwa wanachofanya ni kujaribu kuchunguza tofauti na vikwazo vya usawa wa afya vilivyopo ndani ya mfumo wa carceral kupitia lenzi au mtazamo dhidi ya ubaguzi wa rangi. Pia wanaangalia hali halisi iliyopo katika mchakato wa kutunga sheria na sheria ya awali (HB1470), ambayo ilileta mwanga kuhusu hali ya afya ndani ya Kituo cha Kizuizi cha Kaskazini Magharibi. Sheria hiyo inaruhusu nafasi ya kutathmini jinsi ya kupanga mikakati, kupanga, na kushinikiza utungaji wa sheria zinazolingana. Cyril alibainisha kuwa wengi wa wanachama wa

Kikundi cha Kazi wana uzoefu wa maisha, na kwa sababu hiyo, wako kwenye mstari wa mbele kutetea mabadiliko. Cyril alimaliza maelezo yake mapya kwa kusisitiza ya kwamba usawa wa afya upatikane kila sehemu.

**Kikundi cha Kazi cha Mahitaji ya Kitendaji cha Ufikiaji wa Ulemavu (D-AFN)**

- Viongozi wenza: Todd Holloway, Yen Baynes (DOH), na Tara Bostock (DOH)
- Matukio ya Mkutano: Jumatatu ya Pili ya kila mwezi saa 4:30-6:00 jioni na Jumatatu ya Nne ya kila mwezi saa 4:30-5:30 jioni
- Maelezo ya Kikundi cha Kazi:

Todd alibainisha kuwa kazi ya kikundi haibadiliki na pia alielezea mambo haya yanayofuata:

  - Todd na Keshreeyaji Oswal walitoa wasilisho kuhusu Harakati Huru ya Maisha. Wasilisho uliguzia historia (harakati ilikuwepo tangu mwishoni mwa miaka ya 1960 na ilikuja wakati wa sheria ya Haki za Raia na kuundwa kwa Sheria ya Urekebishaji mnamo 1973). Todd alidokeza kuwa DOH na Jimbo la Washington zinatoa mfano mzuri kote nchini.
  - Dean Sydnor kutoka kundi la Hopelink's RARET aliripoti juu ya matokeo ya zoezi la mezani la Mtandao wa Watoa Huduma za Usafiri wa Dharura (ETPN).
  - Tangu hivi majuzi, kundi linafanya kazi na Yen na Tara kutoka DOH ili kupanua mipango ya ushiriki na ujumuishaji wa ajira katika 2024 (kundi kinatayarisha kampeni ya mitandao ya kijamii).

**Majadiliano/Maoni**

Wahudhuriaji wa mkutano walishiriki mawazo yao katika Gumzo au Chat.

- Todd alishiriki: “Sisi (Kikundi cha Kazi cha D-AFN) tunatoa nafasi kidogo kwa ajili ya upanuzi na uajiri kwa 2024. Ninashukuru kwamba uko pamoja na sisi!”
- Muhudhuriaji mwingine alipongeza msisitizo wa wawasilishaji kuhusu “uwakilishi katika ngazi zote ndio unaoturuhusu kufanya mabadiliko yanayohitajika.” Wahudhuriaji wengine walikubali maoni hayo.
- Wahudhuriaji wengi wa mkutano walitoa shukrani kwa viongozi wote wa Kikundi cha Kazi na kwa mambo muhimu yaliyowasilishwa.

## Mshiriki wa Mawazo na Tafakari ya Mwanchama wa Ushirikiano

Baada ya maelezo mapya ya Vikundi 3 vya Kazi, wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya walishirki tafakari yao.

- Elizabeth Perez alishukuru kila mtu kwa kufanya kazi na DOH kuanzia wakati wa janga.Alitoa shukrani kwa wote wanaoendelea kufanya kazi na DOH na kudumisha uaminifu wa DOH na kuwa waaminifu kwa dhamira yao ya kuhakikisha usawa kwa wote. Aliwahimiza wote kuendelea na kazi, na alibainisha kuwa Ushirikiano umefanya kazi ya

DOH kuwa bora zaidi na wafanyakazi wa DOH watumishi bora kwa Jumuiya.Alikubali kwamba bado kuna nafasi ya kukua.Alibainisha kuwa Idara haiwezi kuhudumia jamii ikiwa haijui jamii inahitaji nini.Alibainisha kuwa kuendelea mbele, wafanyakazi wa DOH wataendeleza kazi na kujitolea kukua.Alidokeza kuwa programu na kazi zinazofanywa na DOH zinawanufaisha wanachama wa Ushirikiano na jamii wanazozihudumia, na akawataka wanachama wa Ushirikiano kufikiria jinsi ya kukua, jinsi ya kufikia jamii na idadi ya watu ambao bado hawajafika mezani, na kujumuisha wengine (washirika wa jumuiya na watu binafsi) kuja kutajirisha na kuendeleza kazi zao kuhusu maono ya usawa kwa wote.

- Todd alibainisha kuwa alishiriki mifano michache katika Chat na kuhimiza kila mtu kusoma wakati ananafasi. Aliwahimiza watu wote kusonga mbele na kutumia sauti zao. La sivyo, wanaowawakilisha wataumia. Alisema.

- Mulki Mohamed alishiriki kwamba katika miaka michache iliyopita, aliona mabadiliko katika Ushirikiano wa Jumuiya. Wakati wa janga watu walikuwa na muda zaidi wa kujiunga na mikutano ya mtandaoni na kujihusisha; hata hivyo, ushiriki umebadilika baada ya janga. Alipendekeza kutafutwa kwa njia zingine za ushiriki. Kwa mfano, ikiwa watu hawawezi kushiriki katika mikutano au Vikundi vya Kazi, labda Ushirikiano unaweza kushirikiana nao kupitia barua pepe, tafiti au miundo mingine. Pia alitoa shukrani kwa washirika ambao wanaongoza pamoja na wanahusika na vikundi vya kazi.
    - JanMarie alikubali na kuongeza kuwa kulikuwa na njia za ufadhili ambazo zilienda kwa jamii kwa njia tofauti wakati wa janga lakini hazitakuwa sehemu ya siku zijazo.

- Ala Talo alionyesha shukrani kwa subira na mwongozo wa timu ya DOH na akawashukuru Frances na Juliet kwa kutoa mwongozo na kumpa uwezo wa kuwa kiongozi mwenza katika Kikundi Kazi cha NH/PI na kuwezesha mazungumzo ya Ushirikiano wa Jumuiya.
    - JanMarie alitoa maoni kuwa ni jambo la maana sana kujua kwamba wanajumuiya wa Ushirikiano wanasaidina na kujifunza kutoka kwa kila mmoja wao.

    - Frances alikubali maoni ya Ala na kutoa shukrani kwa Washirika wote wa Fikra kwa shughuli zote ambazo wamekamilisha, na kwa mikutano yote ya dharura na shughuli zingine wanazofanya pamoja na majukumu yao ya Washirika wa Mawazo, licha ya ahadi na majukumu yao mengine (kwa mfano, kazi na familia). Frances aliwahakikishia wanajamii kwamba hawahitaji kuhisi kwamba wanahitaji kuja wakiwa wamejitayarisha kabisa na ujuzi na maarifa yote. Aliwahimiza wanachama wa Ushirikiano kuja na shauku na kujitolea kwao, wakijua kwamba kila kitu ambacho Idara na Ushirikiano hufanya kinafanywa kwa lenzi ya haki ya kijamii. Aliongeza kuwa Idara inahitaji uzoefu wa maisha na shauku ya wanajamii, na Idara itatoa msaada na chochote kingine kinachohitajika ili kuhakikisha kuwa wanachama wanaweza kutanguliza bidii yao bora. Ikiwa kuna mtu yeyote

angependa kujua jinsi ya kuwa Mshirika wa Mawazo, tafadhali wasiliana na Frances kwa Frances.Limtiaco@doh.wa.gov.

- JanMarie alipongeza maoni ya Ala na maoni ya Frances. Alibainisha kuwa jamii zenye afya zinasaida ukuaji na kujifunza kwa kila mmoja, na kwamba Ushirikiano wa Jumuiya ni dalili ya jambo hilo, ambalo ni mafanikio yenyewe.
- Cyril alishiriki zaidi tafakari yake kuhusu 2023 na nini kitakachomfikisha yeye na Kikundi Kazi katika 2024. Akitafakari mwaka wa 2023, alibaini kuwa imekuwa ya kuvutia kuona idadi kubwa ya kazi iliyohusika, sehemu nyingi tofauti za ushiriki katika viwango tofauti, na miunganisho kati ya juhudi zote. Alibainisha kuwa kwa kuangalia vipengele vyote vinavyohusika na mambo yote tofauti ambayo jamii zinyafanya, inamfanya afikirie ubaguzi kwa kuwapendelea wanao nguvu mwilini, ubaguzi kulingana na jinsia, umri, jinsi mambo haya yanavyoathiri usawa wa afya na kazi zinazohusiana, na jinsi ubinadamu na ukombozi unavyofungamana na kila mmoja. Cyril alibaini kuwa mwaka wa 2023 kulikuwa mambo mengi alojifunza kutokamana nayo na yakamsaidia kukua kwake kiujuzi. Kuhusu nafasi hiyo, Cyril alieleza kuwa wametoka mbali lakini bado kuna safari ndefu mbele yao. Alieleza kuwa ana matumaini kwa mustakbali wa nafasi hii, na kwamba anatazamia kuona watu wengine wakiingia katika nafasi hii na kuhisi kuungwa mkono na kuwezeshwa kufanya kazi yao. Kuhusiana na kazi ya Mkakati wa Momentum Strategy na Elevating Black Wellness (mkakati wa kuboresha afya ya watu weusi), alibainisha kuwa imekuwa ya kuvutia kuwa sehemu ya nafasi hiyo na kuona kile ambacho watu wanakifanya. Cyril alisisitiza umuhimu wa kuwa na nafasi kama hizo na akaangazia kazi ya Can A Brotha Heal na Momentum Strategies.Alibainisha kuwa vyombo vya dola vinapotengeneza njia kwa jamii kutumia uwezo wa jumuiya na kutengeneza mambo kwa njia ya msingi na ya kikaboni ili kukidhi mahitaji ya jamii, basi jamii inatambua kuwa kwa pamoja yanatosha kabisa.Kufikia 2024, alieleza kuwa ametiwa moyo na kazi wanayofanya na Kundi la Jamii ya Wafungwa Weusi, ambalo hivi majuzi lilikuwa na mafungo ambapo walijadiliana na kuchunguza kile kinachoonekana kukuwa katika jamii na kati yao.Cyril alibainisha kuwa anatazamia pia kukaribisha mwanamkakati mpya na Washirika wa Mawazo, na viongozi wapya wa jamii kwa Ushirikiano, akijua kwamba kumekuwa na msingi thabiti uliowekwa kwa uwezekano wote.

    - Christina Blocker alishiriki viungo vifuatavyo yaani *links* katika sehemu ya Gumzo au *Chat*:
        - Cheza tena tukio la Can A Brotha Heal: https://www.elevateblackwellness.com/registration

- JanMarie alimpongeza Cyril kwa kazi yote ambayo anajihusisha nayo na akakubali kwamba kazi nyingi inahitajika katika masuala ya Vijana Wasiokuwa Wazungu, elimu, ajira, na kuhusu kazi ya kupinga ubaguzi wa rangi na mfumo wa haki ya jinai. JanMarie alihimiza kila mtu kujua mengi kuhusu mpango wa Inua Afya Njema ya Watu Weusi au Elevate Black Wellness: https://www.elevateblackwellness.com/

- Frances alitoa shukrani kwa Washirika wote wa Mawazo ya Ushirikiano wa Jumuiya: Lin Crowley, Mayra Colazo, Megan Veith, Pa Ousman Joof, Todd Holloway, Jo Anderson, Cyril Walrond, Lua Pritchard, Kathleen Wilcox, Mulki Mohamed, Van Kuno, Toni Lodge, Jan-Marie Ward, Ahmed Ali, Amelia Bai, Shalom Agtarap, Miranda Vargas, Vincent Perez, Steve Bader, Skye Raphael Rozon, Chaune Fitzgerald. Kwa wanachama wa Ushirikiano ambao wangependa kujifunza jinsi ya kuwa Mshirika wa Mawazo, Frances aliwahimiza wawasiliane naye kwa: frances.limtiaco@doh.wa.gov.
    - Jim House alijibu: "Nihesabu mimi – ninafuraha kufanya kazi na Todd na wengine."
    - Lika Smith alijibu: "Bodi ya Afya ya PI ingependa kujumuishwa kama mshirika wa mawazo."

## Kufungwa kwa Kikao na Hatua Zitakazofuatia

Kwa kumalizia, Amelia aliishukuru timu ya KAI na timu ya DOH kwa usaidizi wao; wanachama wa Ushirikiano kwa ushiriki wao unaoendelea, maoni, mwongozo, na kwa kuhakikisha kuwa majadiliano yote yana lenzi ya haki ya kijamii au mtazamo wa haki ya kijamii; Washirika wa Mawazo kwa mwongozo wao na maelekezo ya kimkakati; na kila mtu kwa kuhudhuria Kikao. Alibainisha kuwa taarifa zote zinazohusiana na Kikao cha leo zitashirikiwa na wanachama wa Ushirikiano wa Jumuiya kupitia Tovuti ya Ushirikiano wa Jumuiya (*Portal*).

**Shughuli:** Timu ya KAI itawatumia wahudhuriaji wote wa mkutano barua pepe yenye kiungo cha madokezo ya mkutano kwenye Tovuti ya WA Portal.

Kikao Kinachofuatia cha Ushirikiano wa Jumuiya kitafanyika: Januari 17, 2024

## Maelezo ya Mawasiliano ya Ushirikiano wa Jumuiya:

Kwa maswali zaidi, maoni, au mazingatio, tafadhali wasiliana na Ushirikiano wa Jumuiya kupitia community.collaborative@doh.wa.gov.

Kwa mawasiliano ya ziada ungana nao:

- Juliet Kwakye, Mratibu wa Uhamasishaji wa Mawasiliano ya Usawa wa Afya kupitia Juliet.Kwakye@doh.wa.gov
- Frances Limtiaco, Uwekezaji wa Jamii na Meneja wa Ushirikiano kupitia Frances.Limtiaco@doh.wa.gov

Tafadhali tembelea tovuti ya Ushirikiano wa Jumuiya ya DOH ili kupata tarehe, maelezo ya mkutano uliopita, mawasilisho, na maandishi mengine ya mkutano.

- Ili kupata madokezo ya mkutano uliopita, chagua kichupo cha Mikutano kwenye ukurasa mkuu. Vidokezo vya mkutano vitawekwa kwenye tovuti ya WA Portal ndani ya wiki mbili baada ya Kikao cha Ushirikiano wa Jumuiya.

## Kumalizika kwa mkutano

Mkutano ulimalizika 5:10 jioni.